# Mchango wa Lugha Asili za Wabantu katika Kuendeleza Historia ya Lugha ya Kiswahili

**Abel Nyamahanga**
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
*nyamahangaa@yahoo.com*

***Ikisiri***

*Makala haya yamechunguza mchango wa lugha asili za Kibantu katika kuendeleza historia ya lugha ya Kiswahili. Makala haya ni matokeo ya kuwepo kwa hoja za wataalamu mbalimbali zinazosigana kuhusu Ubantu wa lugha ya Kiswahili. Uchunguzi, katika makala haya, umefanywa kwa kujikita katika misingi ya ushahidi wa kiisimu. Ushahidi wa kiisimu umefanyika kwa kuzingatia uchunguzi wa lugha ya Kiswahili katika mfumo mzima wa historia ya mgawanyiko wa kusambaa kwa lugha za Kibantu. Ushahidi wa data za kiisimu umerejelewa kwa kuzingatia mwachano na umbali wa kijiografia baina ya jamiilugha moja na nyingine kutoka katika baadhi ya lugha za Kibantu kutoka nchini Tanzania, Zambia na Burundi ili kuthibitisha Ubantu wa lugha ya Kiswahili. Data za msingi za makala zilikusanywa kwa mbinu za uwandani na maktabani. Mbinu ya mahojiano ilitumika kupata data za msingi. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua na kuthibitisha data za msingi yalipatikana kwa mbinu za usomaji wa nyaraka zilizopo maktabani na mtandaoni. Makala haya yanahitimisha kuwa Kiswahili ni mojawapo ya lugha katika jamii kubwa ya lugha za Kibantu.*

**Maneno Muhimu**: Kiswahili, Lugha za Kibantu, Isimu-Linganishi, Isimu-Historia na Ushahidi wa Kiisimu.

## 1.0 Utangulizi

Hapana shaka kuwa watu wengi wanaeleza kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili ni Kibantu, lakini kuhusu lini na wapi lugha hii ilianzia ni suala linalozua mjadala kwa muda mrefu miongoni mwa wataalamu wa lugha hii. Baadhi ya wataalamu wanadai kwamba lugha ya Kiswahili ilitokana na pijini iliyokuwa na athari kubwa ya msamiati wa Kiarabu; ilhali wengine wanadai kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu (Chittick, 1974; Freeman-Greenville, 1959; Hudson, 1985). Kuhusu chimbuko lake, wataalamu wengi wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ilianzia sehemu moja, kisha ikasambaa katika maeneo mengine ya Upwa wa Afrika ya Mashariki. Kusigana huko hakutazamwi tu kama hatua mojawapo ya misingi ya kukua na kukomaa kwa maendeleo ya lugha ya Kiswahili, bali huibua maswali mengi yanayokosa majibu yanayohitaji kuthibitishwa kisayansi.

Ipo mitazamo ya namna mbili inayoelezea uwezekano wa mahali ilipoanzia lugha ya Kiswahili. Kwanza, upo mtazamo unaoeleza kwamba lugha ya Kiswahili ilianza miaka kadhaa kabla ya miaka 100 AD. Mtazamo wa pili unaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ilianza baada ya miaka 100 AD (Gray, 1962; Greenberg, 1963; Sasson, 1980). Kulingana na mitazamo hiyo, inawezekana mtazamo wa pili unatosheleza kwani wanaakiolojia na wanaisimu wanaeleza kuwa Wabantu walifika Pwani ya Afrika Mashariki baada ya miaka 100 AD. Chimbuko la lugha ya Kiswahili linaweza kuhusishwa na Ubantu kwa kuwa kabla ya 100 AD hapakuwa na Wabantu katika Pwani ya Afrika Mashariki (Gray, 1962; Guthrie, 1967; Knappert, 1979). Watalaamu, hasa wanahistoria wanahitilafiana kuhusu nafasi ya lugha za asili katika historia, kukua na kukomaa kwa lugha ya Kiswahili. Makala haya yamechunguza mchango wa lugha za

asili za Wabantu katika kuendeleza historia ya lugha ya Kiswahili.

## 2.0 Mbinu na Upeo wa Uchunguzi

Katika taaluma ya fasihi na lugha, baadhi ya masuala yanayoibua mjadala endelevu miongoni mwa wataalamu wengi ni kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wataalamu walioshughulikia suala hili ni pamoja na Allen (1993), Chiraghdin (1974), Massamba (2002), na Nurse na Spear (1985). Wataalamu hao wanasigana kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili. Tatizo kubwa la wanahistoria hao ni kuwa hawakuzichunguza kwa kina lugha za asili walizozikuta, hasa kuhusu nafasi yake katika historia ya chimbuko na maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Makala haya, hata hivyo, yamelishughulikia suala hilo kwa kuchunguza mchango wa lugha za Kibantu katika kuendeleza historia ya lugha ya Kiswahili. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika katika urejelezi wa baadhi ya lugha za Kibantu kutoka nchini Burundi, Tanzania na Zambia ili kuthibitisha Ubantu wa lugha ya Kiswahili. Data za msingi za makala haya zilikusanywa kwa mbinu za uwandani. Mbinu ya mahojiano ilitumika kupata taarifa zilizokuwa zimelengwa. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua na kuthibitisha data za msingi yalipatikana kwa mbinu za usomaji wa nyaraka mbalimbali.

## 3.0 Mchango wa Lugha Asili za Kibantu katika Kuendeleza Lugha ya Kiswahili

Msimamo wa makala haya ni kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Msimamo huu unatokana na ukweli kwamba lugha ya Kiswahili imefanyiwa utafiti na uchambuzi na wanataaluma kadhaa kwa madhumuni ya kuiainisha katika misingi ya kisayansi. Mtazamo huu unashadadiwa na Chiraghdin na

Mnyampala (1977), Hollingsworth (1966), na Massamba (2007) wanaoeleza kuwa kiisimu, lugha ya Kiswahili ni zao kamili la lugha za Kibantu. Mwanataaluma Malcon Guthrie kutoka Chuo Kikuu cha London, Uingereza alitumia miaka 20 kuchunguza uhusiano uliopo baina ya lugha za Kibantu katika eneo lote la Kusini mwa Jangwa la Sahara (Guthrie, 1970; Tuli, 1985). Guthrie alifanya uchunguzi wa mashina ya maneno 22,000 kutoka lugha 200 za Kibantu. Katika uchunguzi wake, Guthrie alibaini kuwa mashina 2,300 yamezagaa katika lugha mbalimbali za Kibantu na Kiswahili kikiwemo. Mashina 500 yalilingana katika lugha zote 200 za Kibantu. Katika baadhi ya lugha hizo 200 zilizofanyiwa uchunguzi, lugha ya Kiswahili ilionesha kuitikia ulinganifu sawa na lugha ya Kikongo kwa asilimia arobaini na nne.

Ikumbukwe kuwa katika uchunguzi huo, mbinu ya isimu-linganishi ilitumika katika lugha za Kiwemba (Zambia), Kiluba (Katanga), Kikongo (Kongo), Kiyao (Tanzania na Msumbiji), Kirundi (Burundi), Kiswahili (Afrika Mashariki), Kisotho (Botswana), Kisukuma (Tanzania), Kizulu (nchini Afrika Kusini), pamoja na Kinyoro nchini Uanda (Guthrie, 1967). Matokeo ya utafiti huo yanapelekea kutoa kauli kadhaa za msingi kuhusiana na chimbuko la lugha ya Kiswahili. Mashina mengi ya lugha ya Kibantu yapo Afrika ya Kati, hasa sehemu zinazouzunguka Mkoa wa Katanga huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kupungua kadiri unavyoelekea mbali nao. Hapana shaka kuwa, Wabantu walienea kutoka sehemu hizo na kusambaa sehemu mbalimbali, zikiwemo zile za Afrika Mashariki. Kufuatana na matokeo ya utafiti huo, ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili ni ya Kibantu.

Mbinu ya isimu-linganishi imetumika katika makala ili kulinganisha lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Miongoni mwa lugha zilizopewa nafasi katika makala haya ni lugha ya Kinyakyusa na Kigogo (Tanzania), Kichewa (Zambia) na Kirundi (Burundi) ili kuchunguza nafasi ya lugha asili katika kuendeleza historia ya lugha ya Kiswahili. Uteuzi wa lugha hizi ulizingatia kigezo cha umbali wa kijiografia uliopo baina ya jamiilugha moja na nyingine. Vigezo vilivyozingatiwa katika ulinganishaji ni msamiati wa msingi wa lugha za Kibantu. Msamiati wa msingi kwa kawaida haubadiliki kirahisi tofauti na msamiati wa kiutamaduni na ule wa maendeleo ya sayansi na teknolojia (Hassan, 2017). Msamiati wa msingi unahusisha shughuli za kila siku, vitu vya asili na majina ya sehemu za mwili. Vigezo vingine vilivyotumika ni uhusiano uliopo kati ya lugha ya Kiswahili na za Kibantu katika vipengele vya kimofolojia na kifonolojia kama ilivyobainishwa katika sehemu inayofuata.

## 3.1 Msamiati wa Msingi

Msamiati wa msingi wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu unafanana kabisa. Kimsingi, msamiati wa msingi ni ule unaohusu mambo, ambayo hayabadiliki badiliki kutokana na mabadiliko ya utamaduni, tofauti na msamiati mwingine unaotumika katika mazingira mengine, hasa ya kiutamaduni (Besha, 1994; Khamisi na Kiango, 2002). Katika msamiati wa msingi, tofauti zinaweza kujitokeza katika matamshi au mabadiliko kidogo ya viambishi vyake, lakini si katika mzizi. Tunapolinganisha msamiati wa msingi wa lugha ya Kiswahili na wa lugha nyingine za Kibantu tunabaini kuwapo kwa mfanano ulio wazi. Data katika Jedwali la 3.1 zinaonesha msamiati wa msingi katika lugha ya Kiswahili, Kinyakyusa, Kigogo, Kichewa na Kirundi.

**Jedwali 3.1: Msamiati wa Msingi wa Lugha za Kibantu**

| # | Kiswahili | Kichewa | Kigogo | Kinyakyusa | Kirundi |
|---|---|---|---|---|---|
| **A** | Jino | *Dzino* | *Lino* | *Lino* | *Irinyo* |
| **B** | Cheka | *Seka* | *Seka* | *Seka* | *Guseka* |
| **C** | Kula | *Kudya* | *Kulya* | *Kulya* | *Kurya* |
| **D** | Moto | *Moto* | *Moto* | *Moto* | *Umuriro* |
| **E** | Lima | *Limani* | *Lima* | *Lima* | *Rima* |
| **F** | Mwana | *Mwana* | *Mwana* | *Umwana* | *Umwana* |

Data, katika Jedwali la 3.1, zinaonesha mfanano mkubwa wa msamiati wa msingi baina ya lugha teule za Kibantu na lugha ya Kiswahili. Aidha, tofauti ipo katika baadhi ya maneno. Kwa mfano, katika namba D, neno *umuriro* katika lugha ya Kirundi hutofautiana na lugha nyingine. Pia, katika namba E neno *limani* katika lugha ya Kichewa linatofautiana kidogo na maneno mengine. Tofauti hizo zinaweza kusababishwa na lugha hizo kutaka kujitofautisha na lugha nyingine ama kutokana na mwachano wa umbali wa kijiografia. Mifano iliyooneshwa katika Jedwali 3.1 inathibitisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu.

## 3.2 Mofolojia ya Maneno ya Kibantu

Kimofolojia, lugha za Kibantu zina mfanano mkubwa unaojidhihirisha katika maumbo ya maneno. Nomino asilia za Kiswahili zina miundo ya kiambishi ngeli na shina (Matei, 2004; Rubanza, 2003). Miundo hiyo imebainishwa katika Jedwali la 3.2 la mofolojia ya nomino za Kibantu. Muundo huu wa nomino unajitokeza pia katika lugha nyingine za Kibantu, ambapo kiambishi ngeli hutanguliwa na kiambishi kitangulizi kama inavyojipambanua katika ulinganishi wa maumbo katika nomino za msingi baina ya Kiswahili na lugha teule za Kibantu.

Mifano katika Jedwali la 3.2 na Jedwali la 3.3 inaonesha mofolojia ya nomino na vitenzi mtawalia.

**Jedwali 3.2: Mofolojia ya Nomino za Kibantu**

| # | Kiswahili | Kichewa | Kigogo | Kinyakyusa | Kirundi |
|---|---|---|---|---|---|
| **A** | **Ji**-no | ***Dzi***-*no* | ***Li***-*no* | ***I-li***-*no* | ***I-ri***-*nyo* |
| **B** | **M**-kono | ***N***-*kono* | ***Mw***-*oko* | ***I-ki***-*boko* | ***U***-*ku-boko* |
| **C** | **M**-oto | ***M***-*ito* | ***M***-*oto* | ***U-m***-*oto* | ***U***-*mu-riro* |
| **D** | **M**-tu | ***Mu***-*nthu* | ***Mu***-*nu* | ***U-mu***-*ndu* | ***U***-*mu-ntu* |
| **E** | **Mw**-ana | ***Mw***-*ana* | ***Mw***-*ana* | ***U-mw***-*ana* | ***U-mw***-*ana* |

Data zinaonesha kwamba nomino za Kiswahili zina muundo wa kiambishi ngeli na shina. Muundo huu unajitokeza pia katika lugha za Kibantu za Kichewa, Kigogo, Kinyakyusa, na Kirundi. Katika mifano hii, maumbo yaliyokolezwa wino mzito ni viambishi vya ngeli. Katika lugha za Kigogo, Kinyakyusa na Kirundi kiambishi ngeli katika baadhi ya nomino hutangaliwa na kiambishi awali //i-// na //u-//.

**Jedwali 3.3: Mofolojia ya Vitenzi vya Kibantu**

| # | Kiswahili | Kichewa | Kigogo | Kinyakyusa | Kirundi |
|---|---|---|---|---|---|
| **A** | Ku-l-**a** | *Ku-dy-**a*** | *Ku-ly-**a*** | *Ku-ly-**a*** | *Ku-ry-**a*** |
| **B** | Ku-chez-**a** | *Ku-vin-**a*** | *Ki-dawal-**a*** | *Ku-kin-**a*** | *Ku-vyin-**a*** |
| **C** | Ku-chek-**a** | *Ku-sek-**a*** | *Ku-sek-**a*** | *Ku-sek-**a*** | *Gu-sek-**a*** |
| **D** | Ku-lim-**a** | *Ku-liman-**i*** | *Ku-lim-**a*** | *Ku-lim-**a*** | *Ku-rim-**a*** |

Data, katika Jedwali la 3.3, zinaonesha kuwa vitenzi vya lugha ya Kiswahili vyenye asili ya lugha ya Kibantu huishia na irabu **a**. Muundo huu unajitokeza pia katika lugha za Kibantu za Kichewa, Kigogo, Kinyakyusa, na Kirundi. Aidha, tofauti ipo katika baadhi ya maneno. Mathalani, katika namba D, neno *ku-liman-i* katika lugha ya Kichewa limeishia na irabu **i**. Mofolojia

ya vitenzi vya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu inafanana.

### 3.3 Mfuatano wa Vipashio vya Lugha ya Kibantu

Mfuatano wa vipashio katika sentensi za lugha ya Kiswahili na lugha teule za Kibantu ni kiima (K), kitenzi (T) na yambwa (Y), ambavyo vinaweza kuwa kimoja na zaidi (Hebwe na Karanja, 2004; Mgullu, 1999; Waihiga, 1999). Mfuatano wa vipashio vya lugha ya Kibantu umeoneshwa katika Jedwali la 3.4. Jedwali la 3.4 linaonesha mfuatano wa vipashio vya lugha ya Kiswahili, Kinyakyusa, Kigogo, Kichewa, na Kirundi katika sentensi.

**Jedwali 3.4: Mfuatano wa Vipashio vya Lugha za Kibantu**

| Lugha | Kiima | Kitenzi | Yambwa | Sentensi |
|---|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | Mtoto | Anakula | Ugali | Mtoto anakula ugali |
| **Kichewa** | *Mwana* | *ukudya* | *Usima* | *Mwana ukudya nsima* |
| **Kigogo** | *Mwana* | *Ukulya* | *Ugali* | *Mwana ukulya ugali* |
| **Kinyakyusa** | *Umwana* | *Ukulya* | *Ikyindi* | *Umwana ukulya ikyindi* |
| **Kirundi** | *Umwana* | *ukurya* | *ubugari* | *Umwana ukurya ubugari* |

Data, katika Jedwali la 3.4, zinaonesha kuwa mfuatano wa vipashio katika sentensi ya kawaida katika lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu ni wa kiima (K), kitenzi (T) na yambwa (Y). Kwa mujibu wa zilizooneshwa, mofolojia ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu hufanana. Ushahidi huu

unathibitisha na kudhihirisha wazi kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Kwa hiyo, mjadala kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili haiwezi kufanywa bila kuhusisha ushahidi wa kiisimu baina yake na lugha za Kibantu.

## 4.0 Hitimisho na Mapendekezo

Kwa ujumla, uchunguzi wa lugha yoyote hauna budi kuhusisha misingi ya utafiti wa vipengele vya isimu-linganishi, isimu-historia, mijongeo pamoja na mwachano na makutano ya jamii za inayochunguzwa (Bright, 1965; Chami, 1994; Msanjila, 2006). Uchunguzi kuhusu lugha ya Kiswahili unapaswa kuhusisha eneo lote la Kusini mwa Jangwa la Sahara ili kubaini mchango wa lugha asili za Kibantu katika historia ya lugha ya Kiswahili. Kwa kurejelea mifano iliyooneshwa, makala yamethibitisha kuwepo kwa mchango mkubwa wa lugha asili ya Kibantu katika kukuza na kuendeleza historia ya lugha ya Kiswahili. Mtazamo huo unathibitisha ubantu wa lugha ya Kiswahili, hasa ukichunguza vigezo vya kimiundo na ulinganishi. Jambo linalokubalika ni kwamba jamii na tamaduni za binadamu pamoja na lugha zao huathiriana. Athari za mwingiliano huo huwa ni suala changamano mno kiasi kwamba, hazipaswi kupuuzwa katika uchunguzi wa nafasi ya lugha asili za Wabantu katika historia ya lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, ulingano uliojidhihirisha katika mifano iliyobainishwa unaonesha kuwa Wabantu walitamalaki na kuzagaa katika eneo lote la Kusini mwa Jangwa la Sahara, na walikuwa na mwingiliano na jamii nyingine katika nyanja za kibiashara na kiutamaduni. Mwingiliano huo ulisababisha lugha zao kuathiriana, kufanana na kutofautiana kulingana na umbali wa kijiografia kati ya jamii moja na nyingine.

## Marejeleo

Allen, J. D. V. (1993*). Swahili origins: Swahili culture and Shungwaya phenomenon*. Athens: Ohio University Press.

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa isimu na lugha*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Bright, W. (1965). *Socialinguistics.* Mouton: The Haque.

Chami, F. A. (1994). *The Tanzania Coast in the first millenium ad: Archeology of the iron-working farming communites.* Uppsala: Societas Archeologica Uppsaliensis.

Chiraghdin, S. (1974). Kiswahili tokea Ubantu hadi ki–standard katika *MULIKA 6,* 57– 61.

Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Chittick, N. (1974). Kilwa: *An Islamic trading city on the East African Coast, Volume 2.* Nairobi: British Institute in East Africa.

Freeman-Grenville, G. S. P. (1959). Medieval evidence for Swahili. *SWAHILI, 29*(1), 10–23.

Gray, J. M. (1962). *A history of Zanzibar: From middle ages to 1856*. London: Oxford University Press.

Greenberg, J. (1963). The language of Africa. In *Kiswahili Journal of American Linguistics Vol. 2.* Philadelphia: Philadelphia University of Pennsylavia Press.

Guthrie, M. (1967). *Comparative Bantu Vol 1*. Farn Borough: Gregg International Publisher.

Guthrie, M. (1970). *Comparative BantuVol 2*. Farn Borough: Gregg International Publisher.

Hassan, F. (2017). Chimbuko la lugha ya Kiswahili: Tathmini ya nadharia tete ya Kaskazini Mashariki ya Kenya. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, *3*, 104–117.

Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Hollingsworth, L. W. (1966). *Historia fupi ya Pwani ya Afrika Mashariki*. London: Macmillan and Co. Limited.

Hudson, R. A. (1985). *Socialinguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Khamisi, A. M., & Kiango, J. G. (2002). *Uchambuzi wa sarufi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Knappert, J. (1979). *Four centuries of Swahili verse: A literary history and anthology*. Nairobi: Heinemann Education Books Ltd.

Matei, A. K. (2008). *Darubini ya Kiswahili, ufafanuzi kamili wa sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa isimu: Fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili origins and the Bantu divergence-convergence theory*. University of Dar es Salaam: Insitute of Kiswahili Research.

Mekacha, R. D. K. (2000). *Isimujamii: Nadharia na muktadha wa Kiswahili*. Osaka: Osaka University of Foreign Studies.

Msanjila, Y. P. (2006). Nadharia katika isimujamii: Mjadala unaoendelea katika *Mulika*, 27, 40–48.

Nurse, D., & Spear, T. (1985). *The Swahili reconstructing the history and language of African society*. Philadelphia: Philadelphia University of Pennsylavia Press.

Rubanza, Y. I. (2003). *Sarufi: Mtazamo wa kimuundo*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Tuli, R. S. K. (1985). *Chimbuko la Kiswahili, kukua na kuenea katika Afrika Mashariki*. Dar es Salaam: Utalii Exporters and Publications.

Waihiga, G. (1999). *Sarufi fafanuzi ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.